# Yesu ni nani?

*‘kwa maana hatujihubiri wenyewe, bali Kristo Yesu ya kuwa ni Bwana, na sisi wenyewe kuwa tu watumshi wenu…’*

(2 Wakorintho 4:5)

*Peter Walker*
**www.1peter1three.weebly.com**

Nimeandika kitabu kwaajili yako msomaji. Ahsante kwa kuniruhusu kukushirikisha kuhus Yesu Kristo.

Sina utaratibu maalumu wa kufuata kwenye Biblia, wala sina uhakika wapi nasimama kwenye mafundisho mengi ya kibiblia. Lakini najua mimi ni mwana wa Mungu na napenda mafundisho ya Mungu. Niruhusu nikushirikishe ninachofikiria…

## Utambulisho:

**Kama unajiuliza hili swali- ‘Yesu ni nani?’ – upo mahali pa kustaajabika sana!**

Unaweza ukawa na hasira na Mungu au kushindwa hata kumuamini tena katika hichi kipindi. Au labda unamuamini Mungu lakini umemizwa sana. Labda wewe ni Muislamu, Muhindi, Mbudha, au mtu waa Imani nyingine. Unaweza ukawa sehemu nyingine kiujumla hata wewe mwenyewe ukashindwa kuielewa… Hata hivyo Rafiki yangu, vyovyote unavyofikiria, vyovyote unavyojihi au popote ulipo, Mungu wa Biblia kutoka kitabu cha mwanzo mpaka cha mwisho, anakukaribisha kwake hadi ‘anakusihi’ umuulize **‘Yesu ni nani?**’

Unaweza ukawa na maswali mengi ambayo sitoweza kuyajibu baadhi. Lakini kwenye kitabu hiki kidogo, nakuja kwako tu kama ‘muumini’ wa Yesu, na kukushirikisha mawazo yangu. Vyanzo vyangu vikuu ni Imani, Biblia na Roho Mtakatifu.

Naamini ya kuwa Biblia - mkusanyiko wa vitabu 66 ni Neno la Mungu. Kama ilivyo kitu chochote kile kizuri na cha kweli, Biblia nayo inaweza isieleweke, kutumika vibaya au kutoaminika. Ingawa ya kuwepo mapungufu ya kibinadamu katika matumizi ya Biblia, bado inabakia kuwa ni neno la Mungu la ukweli na kuaminika. Iliandikwa na watu ambao hawakufunzwa, ili iweze kuwa rahisi kusomwa. Mungu hajajificha kwetu kwa njia ya Biblia, bali anajidhihirisha kwetu.

Sasa ngoja nikupe mawazo yangu juu ya maswahi yote muhimu: **‘Yesu ni nani?**’

## Yesu ni nani?

Biblia inatufundisha kuwa Yesu Kristo – maana ‘*Bwana anaokoa’* – ni Mungu kwa njia ya binadamu. Mungu alishuka chini kutoka mbinguni kuwa binadamu, ili tuweze kumjua Mungu vizuri’,na kuungana naye kimwili.

Yesu ni Mungu ‘kimwili’. Alikuja kutusamehe dhambi zetu na kutupa uzima wa milele. Huyu ‘ndiye’ Yesu na ‘kwanini’ alikuja duniani.

***Ufunuo:***

Biblia yenyewe inatuambia ni kitabu kisichoeleweka na cha ajabu. Hatuwezi kuamini kirahisi - kuwa Mungu alijigeuza kuwa binadamu ili atuokoe. Hatuwezi kuelewa kabisa, ni kitu kikubwa na cha kushangaza kwetu! Lakini Biblia inatuambia ni ukweli – ukweli wa kustaajabisha – kuweza kukubali kirahisi.

Tunaambiwa kuwa ndio ukweli wa Mungu – Yesu Kristo – ni ‘*Roho na kweli’,* na anakuja kwetu sio kwa ‘kuelewa’ lakini kwa ‘ufunuo’ kwenye roho zetu na mioyo

yetu.

Kama – upo kama mimi na kama watu wengine – kujaribu ‘kumjua’ Mungu au kumuweka akilini mwako, inaweza ikawa vigumu kuleta roho zetu na mioyo yetu kushika usukani. Lakini Rafiki yangu jua yakuwa kila kitu kizuri maishani mwako – Rafiki,familia,furaha, upendo, amani, msamaha, huruma – sio vya ‘kweli’ wa akili bali vya moyo na roho. Kwenye vitu vingi tumeleta akili zetu, uelewa wetu, kuumiza ‘ukweli wa moyo’, au mahusiano. ***Umeshawahi kuleta akili yako itawale moyo wako, na ukaja kujutia?*** Kama Mungu yupo kwenye akili yangu ndogo au hatabiriki ‘kumuelewa’, basi atakua ni Mungu mdogo kweli!

Tunaambiwa kwenye Biblia, ‘Mungu ni roho, na wafuasi wake lazima wamuabudu katika roho na kweli.’ Yesu mwenyewe alisema kwa meneno yake na ufunuo wake, ‘maneno yangu ni roho na uzima.’

***Ushawahi hisi ukweli kuhusu Yesu kuwa changamoto akilini mwako, lakini unagonga mlango wa moyo wako?***

**Ujumbe wa Kristo:**

Inastaajabisha vile Yesu alivyojionyesha kwa watu kwa '*imani'* zao. Hakuja kutupa pesa wala utajiri. Hakuja hata kutoa majibu ya kiimani. Alisema vitu kama, '*kuna mtu yeyote mwenye kiu? Mwache aje kwangu kunywa…yeyote aniaminie mimi, vyanzo vya maji ya uzima vitakua ndani yao.'* Yesu aliuliza kama tuna 'kiu', na akahaidi 'maji ya uzima.' Hii '*haiendani'* kabisa na uchumi wetu wa kila siku; '*haiendani'* na akili zetu. Lakini inashuka ndani ya nafsi zetu na kukutana na mahitaji yetu hata na zaidi.

Je hili swali **la Yesu – 'una kiu? – lipo ndani ya nafsi yako?'**

Au, kwa mfanoYesu akageukia umati wa watu akauliza, '*kuna mtu yeyote mchovu?'* na kaahidi '*pumzika'* vyovyote vile.

Yesu alifanya  miujiza, lakini alikua na sababu maalumu ya miujiza yake. Kuna siku Yesu aliwaambia watukuwa sababu ya kufanya miujiza ni ili tuweze kelewa ya kuwa ana uwezo wa kusamehe dhambi

zetu. Hakufanya miujiza ili tu kufanya Maisha yawe safi kwa baadhi ya watu, kwa mda mfupi. Alifanya miujiza ili tuone uwezo wake wa kusamehe makosa yetu, na *'kuandika majina yetu mbinguni.'*

**Je, ujumbe wake ni upi? Nawezaje kuwa na 'maisha' haya, 'pumziko' hili, 'visima vya maji ya uzima' nafsini mwangu?**

Hapa ndipo ujumbe wa Yesu unakuja maishani mwetu, - kipekee Zaidi…

Yesu alisema, *'Mimi ndio lango, na yeyote apitaye kupitia mimi ataokolewa.'* Yesu hakufundisha kuhusu Mungu; Yesu alitualika kwake tumjue Mungu. Kitu kikubwa ulichonacho maishani mwako sasa hivi ni 'mtu' sio 'kitu' au kujua kitu. Fikiria hivi kwa dakika**. Ni kitu gani cha thamani kwako mwisho wa siku?** Na kuhakikishia ni mtu.  Mungu pia. Ukweli wa ndani wa Mungu kwako -ni yeye mwenyewe.  Dhumuni lake la kuwa binadamu ni ili mimi na wewe tuweze kumuona, kumshika, kumjua vyema. Hivyo basi jina Yesu alilopewa lilikua 'Emmanuel', maana '*Mungu Pamoja*

*nasi.*' Yesu – Mungu kama mwanaume - alikuja ili awe nasi sote, sasa na hata milele.

## Imani:

Yesu anatuimarisha ‘kumwamini’ yeye. Hii ilikua ni ukaribisho wake alivyokua na watu, na kuweza ‘kumuona’ yeye. Kama waliweza ‘kumuona’ kwanini tunashinikizwa ‘kumuamini’ yeye? Vitu viwili vilinijia akilini juu ya suala la ‘Imani’:

**1.Rafiki wa kweli anakuamini!**

Ushawahi kuwa na ‘rafiki’ ambaye sio kwa ajili yako? Huyu mtu anakujua na anakuona, na pia anakupa nafasi yako hata ukiwa Pamoja nae; huyu mtu ana ‘mahusiano’ na wewe, lakini ‘hakamini.’ amefunga kabisa moyo wake kake. ***Unawea ukalinganisha hii hali, hii hisia kwenye mahusiano yako?***

Yesu alikuja – Mungu wa mwili – kuwa na ‘sisi’. Jina lake kabisa, Emmanuel, maana *‘Mungu pamoja nasi’*[1] Yesu hataki tu umjue yeye,; amekuja kuwa na mapenzi, ‘imani’ mahusiano na wewe. *Kuaminiana ni ishara ya urafiki wa kweli.*

---

[1] Isaya 7:14; Mathayo 1:23

Yesu alisema, *'nimekuita wewe rafiki yangu.'* Yesu pia alisema kuwa hakuna njia kubwa Rafiki anaweza akaonyesha upendo wake, kama kujitoa kwa ajili ya Rafiki yake.[2]

**2. Kuona <u>si</u> kuamini.**

Yesu alivyokua Duniani, watu wengi waliona nguvu na uweza wake, lakini hawakumwamini. Labda unapenda, saa nyingine unatamani au unataka kusema, "*kama tu nkiweza 'kumuona' Yesu…"* ukweli ni, wengi – ambao walimuona kwa njia ya kibinadamu na kujionea miujiza yake, hawakuamuanini. Mara nyingi, akifanya miujiza, watu *'walimgeuka'*. Mwishoni, kila mtu ambaye 'alimuona'- wale waliomsikia, kutembea naye, kufurahia maajabu yake na miujiza – walimgeuka na kuwa kinyume naye na kupanga mambo kisirisiri juu yake. Aliuwawa asubuhi katikati ya kila mtu ambaye alishawahi 'kumuona.'

Sasa Yesu anatuita, 'tuamini', kuwa na 'imani', kutokuwa na wasisiwasi.

---

[2] Yohana 15:13-15

Binadamu alipomuona, alimuua. Hatuwezi tukaamni nafsi zetu kufuata na kuwa waaminifu-kwa vile tunavyoviona machoni mwetu. Tunaweza tukawa waaminifu kwa mda, kama wafuasi wake, lakini baada ya muda macho yetu, akili zetu, na mioyo yetu itatuangusha chini na kutofuata tena. Tunaweza hata tukakataa na kwenda kinyume kabisa na kile tulichokiona na kukipenda.

Yesu kuna siku alimuambia Thomaso, mfuasi wake, <u>‘wamebarikiwa wale wanaoamini akini hawajapata kuona.’</u>

Hapa duniani, Yesu anataka ‘tuone’ kwa macho ya mioyo yetu, na kuamini. – kwa kupokea, kufuata, kutii, kuabudu. Yesu anataka mahusiano ya kweli na wewe, urafiki wa kweli! Siku moja tutapita katika rehema na utukufu , ambapo macho yetu yatakua safi na mioyo yetu imara, na tutamuona ‘ana kwa ana’. Lakini kwa sasa, tunaitwa kuamini tu.

***Je, unahisi ‘unamuona’ Yesu kwa macho ya moyo wako ?***

## Hazina:

***Kwanini ni vigumu 'kumuona' na kumuamini Yesu? Kwanini dunia nzima hawamskii na kutomwamini Yesu?***

Nliposoma vitabu vya manabii, nashangazwa na jinsi Mungu anavyofanya kazi. Tokea mwanzo, ingawa Mungu anampenda kila mtu sawasawa, wengine '*walimjua'* Mungu, na wengine hawakumjua. Hivi ndivyo – na itakua – vigumu sisi kuelewa, kutambua, na kuelezea.

Ilikua hivyohivyo Yesu alivyotembea duniani, kuhubiri na kufanya miujiza. Baadhi ya watu walimdondokea miguuni mwake na kusema, '*wewe ni Bwana'* wengine walimtazama kwa dharau, kumuaibisha na kumjaribu ukuu wake. Hii inawezekanaje? Mtu anawezaje kumuona Kristo na kumuona Mungu, na mwingine kumuona Kristo na kumuona kama binadamu wa kawaida? Siwezi elezea kabisa!

Lakini kile nlichokiona maishani kwa Yesu

na mafundisho yake, ni kuwa alijionyesha mwenyewe ndani yake. *Kiundani Zaidi, na kimyakimya*!

Kama mtu ‘alimuona’ Yesu kwa jinsi alivyo – ‘Mungu Pamoja nasi’ – ufunuo ulifika ndani ya moyo wake, na kumbadilisha milele. Lakini kwasababu huu ufunuo ni wa ndani sana, wakweli na wakimya, unatembea katikati yetu bila sisi kujua. Tunachanganywa na kelele nyingi na matamanio ya dunia, mpaka vitu vya kiundani vya Mungu vinatupita.

Yesu alieleza fumbo dogo kuelezea huu ukweli. Alisema, *‘ukuu wa mbinguni ni kama hazina iliyofukiwa ardhini. Mwanadamu alipoipata, aliificha tena, na kufurahia kuuza kile alichonacho na kununua hiyo ardhi.’*[3]

***Unahisi Yesu ni hazina unayoanza kuiona, lakini watu wengi walio karibu yako hawaioni?***

---

[3] Mathayo 13:44

**Damu:**

Habari za Yesu ni za kustaajabisha! Tunaambiwa kuwa Mungu, alikuja kutuokoa na dhambi zetu,'madoa' yetu. Unajua, ule undani kabisa wa dhambi zetu unaachaga mwendelezo wa damu. Damu, chanzo kikuu cha Maisha ya binadamu, inatiririka pale penye maovu, pale penye matusi, pale penye bahati mbaya, pale penye kifo. Wote tunayo mikononi mwetu, moja kwa moja au sio moja kwa moja. Tunaishi kwenye dunia iliyojengwa kwa utumwa na maovu, na wote tumemwaga damu zetu wenyewe au kutoa watu wengine damu kwa kutumia vitu vya watu waliomwaga damu zao. Ni ukweli usiofichika – lakini umwagaji wa damu upo katikati ya giza nene la Maisha yetu, na utengano wetu na Mungu.

Hivyo Yesu anakuja, na kutaka kutuweka huru na dhambi zetu na giza lililotutawala. Anataka kutuweka huru na makosa tunayoumia na tuliyoyafanya. Anataka kuponya na kurudisha kila roho,kila moyo, na hata ardhi tunayoiishi. Tunaambiwa kuwa Yesu amefungua njia

kwa ajili ya ‘*wokovu’* na ‘*msamaha’* wa nafsi zetu. **Yesu alichukua dhambi zetu zote na kuzibeba mwilini mwake, na kufa nazo.** Msatri mmoja wa Biblia unasema hivi: *‘alifanya dhambi kwa ajili yetu’*[4]

Yesu alichukua hatia yangu na aibu yangu kuifanya iwe yake, na kufa nayo. Kufa na dhambi zanu, Yesu alifufuka kutoka kwa wafu, lakini dhambi zangu hazikurudi naye. Aliziacha dhambi zangu kaburini, hivyo kusema. Yesu alichukua dhambi zangu, alikufa nazo, na kurudi na msamaha na Maisha mapya kwa ajili yangu.

Mstari mmoja kwenye Biblia unaelezea hivi: damu ya Yesu ‘*inanena vyema’* kuliko damu ya dhambi zetu.

Kwa sababu hii, tunapomuamini Yesu na kukubali msamaha wake, tunakua tunamshukuru kwa damu hii, ‘damu ya Yesu.’

***Unataka ‘kusafishwa’ kwa damu yake?***

---

[4] 2 Wakorintho 5:21

**Roho:**

Yesu yuko hai! Yupo na yuko mbinguni. Siku moja utakutana naye '*ana kwa ana'*

Lakini Yesu alipokuwa ananena na wafuasi wake ya kuwa hivi karibuni anatarajia kuondoka duniani kurudi mbinguni, aliwaambia wafurahie - wasiwe na huzuni - kwasababu hii inamaanisha '*roho mtakatifu'* atawajia duniani na kuwa *ndani* yao.

Unaona, Yesu alivyokua duniani, alikua kama binadamu tu. Kama Yesu angekua katika kijiji kimoja, inamaana asingeweza kuwa kijiji kingine. Kama Yesu angekua anaweka mkono wake wa amani juu ya mwanadamu mmoja, inamaana asingeweza kuweka kwa mwingine. Alikua kwa njia ya binadamu, hivyo alikua na muda na nafasi ndogo kama tuishivyo.

Yesu alipopaa mbinguni, Roho ya Yesu, Roho wa Mungu, alijaa duniani kote. Hii inamaanisha kuwa mwili na amani ya Yesu inaweza kuwa katika kila Kijiji, na katika mioyo na majumbani kwa kila mtu kwa wakati mmoja. Pia inamaanisha

kuwa Yesu alikuwa na uwezo wa kuishi ndani yetu, sio tu kwa kutembea pembeni yetu.

Sasa kwa vile Yesu ameshamaliza kazi yake hapa duniani – kufa na kufufuka, kutupa msamaha na uzima wa milele – anaishi mbinguni. Tunaungana nae sasa kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Tunapomuamini Yesu, anakuja kwetu kwa njia ya Roho Mtakatifu, na kuishi ndani ya mioyo yetu, roho zetu na nafsini mwetu – ‘Mungu Pamoja nasi.’

***Unataka kumuamini Yesu, na kuwa na Roho Mtakatifu katika moyo wako na maishani mwako?***

**<u>Mwaliko:</u>**

Yesu anasema, *‘mimi ndio lango, yeyote ajaye kupitia mimi ataokolewa*.’ (Yohana 10:9)

***Unataka kumwalika Yesu ndani ya moyo wako na maishani mwako sasa hivi?***

Huu ni uamuzi wa kiroho, na kutoa maisha yako kwa Yesu utapata na msamaha wa dhambi zako, na maisha ya milele. Pale unapokuja kumjua Yesu, unakua kwenye njia mpya, na hii ni ‘*nuru ing’aayo, ikizidi kung’aa hata mchana mkamilifu.’ (Mithali 4:18)*

Hapa ndo ambapo unaweza ukavuka daraja kutoka kwenye kifo kwenda maishani, na kumjua Yesu Kristo. Kuna vitu 2 vya *‘kufanya’.* Nimeviandika hapa chini, na kuandika sala, unaweza isoma na ‘kusali’ kutoka moyoni mwako:

1. **<u>Toba:</u>**

   Utahitajika kutubu dhambi zako. Ndio, hii ni hatua ngumu, lakini ndiyo

ambayo Yesu anahitaji. Unahitaji kuamua sasa kwa msaada wa Mungu utaziacha dhambi zako na njia zake maishani mwako – *tamaa ya hela, tamaa za kimwili, uongo, mazoea, uzinzi, picha za utupu, n.k.*

Kutubu dhambi ni ‘maamuzi ya moyo’, na baada ya muda inapaswa kuonekana maishani na nyumbani kwako. Kuna vitu utahitaji kuviacha, kuwasiliana, kuvitupa, kuvizima, kuvigawa…kama umeamua sasa kutubu, na ‘kugeuka’ (hivi ndio ‘toba’ inamaanisha), unatazamana na njia sahihi kwa hatua ijayo.

**2. <u>Imani kwa Yesu Kristo:</u>**

Tumeongelea hapo juu umuhimu na ‘ukweli’ wa kuamini na Imani katika mahusiano yoyote. Yesu anatuita ‘kumwamini’ yeye, Yesu anatuita kuchukua hii <u>hatua ya Kiimani,</u> na kupaza sauti na kutamka juu ya Imani kwake.

Nimeandika sala hapa chini unaweza ifanya iwe yako. Sala lazima itoke

moyoni mwako, na iwe ya kweli.

Kama unatubu dhambi zako na kuweka Imani yako kwa Yesu, atakuwekea wakati huu Roho Mtakatifu wake moyoni mwako, atasamehe dhambi zako, na kuandika jina lako Mbinguni!

**<u>Sala:</u>**

***Bwana Yesu, nakushukuru kwa kunipenda. Nakushukuru kwa kufa kwa ajili ya dhambi zangu. Nakushukuru kwa kunisamehe na kunipa uzima wa milele.***

***Leo natubu dhambi zangu, na kuweka Imani yangu kwako. Nakuomba unisamehe dhambi zangu, na kumimina Roho Mtakatifu wako ndani yangu.***

***Ahsante, Bwana, kwa kunisamehe. Ahsante, Bwana Yesu, kwa kuniokoa. Nisaidie sasa kuwa mwaminifu, na kukufuata wewe siku zote za Maisha yangu, mpaka nikuone ana-kwa-ana. Kwa jina la Yesu' ninaomba, amen!***

## Maisha mpya:

Kama umechukua hii hatua ya Imani kwa Yesu, umeokolewa! Wewe *ni ‘kiumbe kipya’.* Huu ni ukweli wa Mungu. Huu ni ujumbe kutoka kwa Yesu.

Kama ‘mwamini’ mpya, ni muhimu sana uanze kusoma Bibli kila siku, na kutumia dakika chache kusali. Pia ni muhimu sana kuwa katika kanisa zuri la kikristo, ili uweze kukua kiimani na kupata msaada kutoka kwa waamini wengine.

Kama hauna Biblia, nakusihi utafute moja ununue: **Biblia Habari Njema.**

Ninachokifanya mimi nasoma ukurasa mmoja kila siku. Labda naanza na kitabu cha **LUKA,** na kuendelea kukisoma…

Tafuta kanisa zuri la kuaminika. Sali na muombe Mungu akuongoze kwenye huu uamuzi. Muombe juu ya kanisa, mtu sahihi mkristo analolijua. Hakikisha kufika kanisani mara moja kwa wiki ni lazima, ‘kujitolea’ kwa Bwana. Itakubidi ubadilishe baadhi ya vitu katika ratiba yako, na hata kwenye matumizi yako, ili kufanikisha hili.

*Bwana atakutunuku kwa kufanya hivi!*

Ningependa kusikia kutoka kwako! Kama umeamua kuchukua hatua hii ya kiimani, kupitia tovuti yangu, nitumie barua pepe na unijulishe. Nitafurahia na wewe, na kukuombea!

Ubarikiwe, kaka yangu, dada yangu! Mpaka pale tutakapoonana ana kwa ana – kwenye mkusanyiko wa kifamilia! - Mungu akubariki, akulinde na ufanikiwe kwa jina la Yesu'!

Kwa habari nyingine nyingi tembelea tovuti yangu hapa chini:

**www.1peter1three.weebly.com**

***‘Bwana akubariki, na kukulinda; Bwana akuangazie nuru za uso wake, na kukufadhili; Bwana akuinulie uso wake, na kukupa amani.’***
(Hesabu 6:24-26)

*Vitabu vilivyoorodheshwa:*

**Mungu anatusihi** kuja **kwake:** 2 Wakorintho 5:20

**Kumjua tu Kristo, vitabu vyake, Roho wake:** 1 Wakorintho 2:2-3

**Kuvutiwa na kutoangaliwa vyema kwa Biblia:** Waebrania 4:1-11 na 2 Wakorintho 4:2

**Waandishi wa vitabu bila ujuzi:** Matendo ya mitume 4:13

**Jina Yesu maana yake, 'Bwana anaokoa':** Mathayo 1:21

**Yesu kama Mungu kwa njia ya binadamu:**
Isaya 7:14/Mathayo 1:23; Isaya 9:6; Yohana 1:1-5,9,14; John 14:9; Yohana 9:38/Mathayo 14:33/kutoka 20:5; Yohana 5:46; Wakolosai 1:15-20; Waebrania 1:3; Wafilipo 2:6-11; Zakaria 14:9/Matendo ya mitume 4:12; Ufunuo 1:13-18.

**Kusudi la Yesu kusamehe na kutoa uzima wa milele:** Luka 5:24; Yohana 11:25-26; Yohana 4:13-14

**Ufunuo, vigumu kuelewa!:** Yohana 6:37, 65; Mathayo 16:16-18; Warumi 11:33-36; Isaya 55:8-9; Zaburi 36:9; 2 Wakorintho 4:6; Yohana 4:24 na Yohana 6:63.

**Imani kwa Kristo:** Yohana 7:37-38; Yohana 11:25-26; Yohana 9:35; Mathayo 11:28-30; Luka 5:24; Luka 10:20; Yohana 10:9; Yohana 5:39-40; Yohana 15:13-15.

**Kuona si kuamini:** Yohana 11:4,53; Mathayo 26:56; Marko 15:25; (3 ya asubuhi) Yohana 20:29; 2 Wakorintho 4:6; 2 Wakorintho 5:7; 1 Yohana 3:2; 1 Wakorintho 13:12

**Mungu anatupenda wote sawa!:** 2 Petro 3:9; 1Timotheo 2:4; Mathayo 18:14; Yohana 3:16

**Ufunuo wa Ndani na Wakweli:** Mathayo 16:20; Marko 1:24,34,44; Marko 4:11; Isaya 6:9; 2 Wakorintho 5:16; Zaburi 42:7; Mathayo 13:44

**Damu na uhuru ndani ya Kristo:** Isaya 1:18; Zaburi 25:15; 2 Wakorintho 5:17; Wagalatia 2:20; Luka 4:18/Isaya 61:1; Isaya 42:3; 2 Mambo ya nyakati 7:14; 2 Wakorintho 5:21; Waebrania 9:22; Waebrania 12:24. Yohana 14:1-4; Ufunuo 1:13-18; 1 Wakorintho 13:12; Yohana 14:17,26,28.

**Mwaliko na Maisha mapya:** Waefeso 1:13-14; Wakolosai 1:27; Mithali 4:18; Yohana 5:24; Marko 1:15; Mathayo 3:8; Matendo ya mitume 3:19; Warumi 10:9; Luka 10:20; 2 Wakorintho 5:17; Waebrania 10:25; Zaburi 1; Yoshua 1:9; Waebrania 4:12/2; Timotheo 3:16.